

IDARA YA UHAMIAJI TANZANIA



PASIPOTI MPYA YA KIELEKTRONIKI



**MAELEZO YA KINA KUHUSU
VIGEZO VYA KUPATA
PASIPOTI, VIAMBATO
MUHIMU, MALIPO NA
UWASILISHAJI WA
MAOMBI**

www.immigration.go.tz

UTANGULIZI

Hii ni pasipoti yenye kifaa maalum “Micro-chip” chenye uwezo wa kuhifadhi taarifa za mwenye pasipoti kielektroniki. Pasipoti hii ina mwonekano unaofanana na pasipoti zinazotolewa na Nchi wananchama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na inaweza kutumika Kimataifa. Ada ya Pasipoti hiii ni **Tsh. 150,000/=**.

SIFA ZA MWOMBAJI WA PASIPOTI MPYA YA KIELEKTRONIKI

Sifa za mwombaji wa Pasipoti mpya ya kielektroniki ni kuthibitisha uraia wake pamoja na safari yake kwa kuwasilisha nyaraka au viambato mbalimbali kama vinavyoelezwa hapo chini.

VIAMBATO VYA JUMLA NAVYOTAKIWA

KUAMBATANISHWA:-

- 1.Cheti/Kiapo cha Kuzaliwa cha Mwombaji AU Cheti cha Uraia cha Mwombaji (Certificate of Naturalisation);
- 2.Cheti/Kiapo cha Kuzaliwa cha mmoja wa Wazazi wa Mwombaji AU Ushahidi wa Uraia wa Mmoja wa Wazazi;

3. Kitambulisho cha Taifa cha Mwombaji au cha Mzazi ikiwa Mwombaji ana umri chini ya miaka 18;
4. Cheti au Kiapo cha Ndoa kwa Wanawake walioolewa;
5. Barua ya Afisa Mtendaji wa Kata (isipokuwa kwa walioajiriwa)
6. Mwombaji anatakiwa kuwasilisha nakala mbili (02) za picha (Passport Size) zenye rangi ya bluu bahari kwa nyuma.
7. Barua ya kuomba Pasipoti.

VIAMBATO MAHSUSI KULINGANA NA AINA YA SAFARI

A. SAFARI ZA BINAFSI

1. Uthibitisho wa shughuli za mwombaji,
2. Barua ya mwaliko,
3. Idhini ya Mzazi/Mlezi halali kwa Mwombaji aliye chini ya Miaka 18.
4. Barua ya Afisa Mtendaji Kata/Sheha na barua binafsi kwa wasioajiriwa.

B. SAFARI ZA KIKAZI, MIKUTANO, TAMASHA NA KADHALIKA.

1. Barua ya mwajiri/kampuni/shirika,
2. Kitambulisho cha Kazi.
3. Barua ya mwaliko.

C. SAFARI ZA MASOMO

1. Barua ya wito wa shule/chuo,
2. Barua ya mdhamini wa masomo,
3. Uthibitisho wa malipo kwa wanaojitegemea (Private Sponsorship),
4. Idhini ya mwajiri kwa walioajiriwa,
5. Idhini ya mzazi/mlezi halali kwa mwombaji chini ya miaka 18.

D. SAFARI ZA MATIBABU

1. Barua toka kwa Daktari Mkuu wa Serikali, au Barua kutoka kwa Daktari aliyesajiliwa, au Barua ya idhini toka Wizara ya Afya.

E. SAFARI ZA KWENDA KWENYE AJIRA

1. Uthibitisho wa barua ya ajira/Mkataba wa kazi,
2. Nakala ya Kitambulisho cha Mwombaji,
3. Barua ya Mwaliko.

G. SAFARI ZA MICHEZO

1. Barua toka TFF au ZFA au,
2. Barua toka chama chochote kilichosajiliwa rasmi kulingana na aina ya michezo, na
3. Barua ya mwaliko.

H. SAFARI ZA KIDINI

1. Barua ya mwaliko,
2. Barua ya dhehebu linalohusika.

I. SAFARI ZA MABAHARIA

1. Mkataba wa kazi,
2. Kitambulisho cha ubaharia,
3. Vyeti vya ujuzi,
4. Barua toka chama cha mabaharia

NAMNA YA KUJAZA FOMU YA MAOMBI YA PASIPOTI MTANDAONI

1. INGIA KATIKA TOVUTI YA
IDARA: www.immigration.go.tz
KISHA NENDA KATIKA KITUFE
CHA e-SERVICES
2. CHAGUA PASSPORT
APPLICATION FORM;
3. CHAGUA MWOMBAJI ALIYE
TANZANIA (IKIWA UKO NCHINI)
AU MWOMBAJI ANAYEOMBEA
UBALOZINI (IKIWA UKO NJE YA
NCHI)
4. CHAGUA OMBI JIPYA;
5. JAZA TAARIFA ZAKO KWA
UKAMILIFU UKIFUATA
MAELEKEZO NA MPANGILIO
(FORMAT) KATIKA KILA
KIPENGELE.

NB:

Baada ya mwombaji kukamilisha kujaza taarifa zake, atafahamishwa ya kwamba usajili umekamilika na kupatiwa namba ya ombi, na namba ya kumbukumbu ya malipo (control number) na kutakiwa kwenda kulipia malipo ya awali (advance fee) ya Tsh 20,000 ndani ya kipindi kisichozidi saa 48. Mteja anasisitizwa kuingiza namba ya kumbukumbu ya malipo kwa usahihi wakati wa kufanya malipo.

JINSI YA KULIPIA FOMU YA PASIPOTI KWA NJIA YA SIMU, INGIA KWENYE MENU YA M-PESA/TIGOPESA/AIRTEL MONEY

(*150*00#/*150*01#/*150*60#)

1. Bonyeza Namba 4 (Lipa kwa M-Pesa) – VODA AU Bonyeza Namba 4 (Kulipia Bili) – TIGO AU Bonyeza Namba 5 (AIRTEL)
2. Bonyeza 4 (VODA) AU Bonyeza 3 Ingiza Namba ya Kampuni – TIGO AU 4 (AIRTEL) Ingiza Namba ya Biashara
3. Ingiza Namba (001001)

Utapata Meseji kwenye Simu kama muamala umekubalika; na kisha

Utapata meseji kutoka kwenye Mfumo **Namba 15200** kama muamala umekubalika;

Mteja atatakiwa kurudi katika tovuti na kubofya **OMBI**

LINALOENDELEA:

Kisha ataingiza **NAMBA YA OMBI** na **NAMBA YA RISITI** au **CONTROL NUMBER**

Na hapo ataweza kupakua Fomu yake ya Maombi na kuichapisha (print)

Ataiwasilisha Fomu hiyo katika Ofisi ya Uhamiaji .

MSAADA KWA MTEJA

Endapo mteja atahitaji usaidizi wakati wa kujaza fomu yake au kuwa na shida yoyote ya kiuhamiaji anaweza kuwasiliana nasi kwa:

E-mail: info@immigration.go.tz

AU

proznz@immigration.go.tz (Kwa walioko Zanzibar)

Simu: 255-22-2850575/6



**Imetolewa na
Kitengo cha Uhusiano
Idara ya Uhamiaji Tanzania**

www.immigration.go.tz